'Tutaendelea kutengeneza sera rafiki sekta ya mafuta, gesi'

NA MWANDISHI WETU

KAMISHNA wa petroli, Goodluck Shirima, amesema Tanzania imejipanga kuandaa sera rafiki zitakazovutia uwekezaji kwenye sekta ya mafuta na gesi asilia ambazo zitawezesha pia kupata mitaji ya kuendesha sekta kwa ufanisi.

Alisema hayo jijini Dar es Salaam katika kongamano na maonesho ya petroli ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPCE'25) linalofanyika kwa siku tatu jijini Dar es Salaam.

"Katika siku ya pili ya mkutano wa EAPCE'25, tumejadili kuhusu umuhimu wa kuwa na mikataba ambayo ina uwazi, inayotabirika na yenye manufaa kwa nchi na kwa wawekezaji. Benki na taasisi za fedha zipo tayari na zina hamu ya kufadhili miradi hii, sisi kama serikali jukumu letu ni kutengeneza mazingira sahihi kupitia sera zetu na sheria," alisema.

Kuhusu sekta ya mafuta nchini, alisema imeimarika kwani mafuta yapo na yanapatikana kwa bei himilivu na kwamba sasa bei ya kushushia mafuta kwenye bandari zote zinafanana kwa lengo la kupunguza gharama kwa watumiaji.

Kuhusu mkondo wa kati wa petroli, Shirima alisema serikali inaendelea kuwa na miradi ya kimkakati ya usafirishaji mafuta na gesi ambapo Tanzania na Zambia zinafanya mazungumzo ili kujenga bomba jipya la kusafirisha mafuta.

Bomba hilo litasaidia kusambaza mafuta pia katika sehemu ambazo linapita kama vile Morogoro, Njombe na Mbeya.

Aliongeza kuwa, kuna mazungumzo yanaendelea na serikali ya Uganda ili kujenga bomba la kusafirisha mafuta safi kutoka Tanzania kwenda Uganda na pia ujenzi wa bomba la gesi kwenda nchini humo ambalo pia litasambaza gesi sehemu ambazo linapita.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Mkutano huo, Mhandisi Joyce Kisamo kutoka Wizara ya Nishati alisema mkutano huo ambao umeendeshwa kwa mafanikio umehudhuriwa na viongozi wa ngazi mbalimbali kuanzia ngazi ya mawaziri, makatibu na wataalamu wa sekta kutoka nchi sita za Afrika Mashariki.

MAKAMU Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji wa Rufani (Mst) Mbarouk Salim Mbarouk akizungumza wakati akifunga mafunzo ya siku mbili ya watendaji wa uboreshaji wa Daftari kutoka halmashauri zote za mkoa wa Dar es Salaam. (PICHA NA INEC).

THBUB yasifu serikali inavyowawezesha wanawake

NA SAIDA ISSA, DODOMA

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeeleza kuwa inatambua jitihada za serikali na wadau wengine katika kuhakikisha wanawake wanapata haki zao na kuwawezesha kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Hayo yalielezwa na Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji (mstaafu) Mathew Mwaimu, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika kuelekea maadhimisho ya siku ya wanawake Duniani yanayofanyika leo.

Alisema pamoja na jitihada hizo wanawake wanakabaliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo vitendo vya ukatili wa kijinsia na uwezo mdogo wa kushiriki shughuli za kiuchumi na kisiasa.

"Kutokana na changamoto hizo, THBUB inapendekeza yafuatayo: serikali iendelee kuwawezesha wanawake kiuchumi na kisiasa ili kuleta usawa katika jamii, serikali na wadau wengine waendelee kutoa elimu itakayowasaidia wanawake kutambua haki zao na kuzidai zinapovunjwa," alisema.

Mapendekezo mengine jamii kuendelea kuzingatia sheria, haki za binadamu na misingi ya utawala bora ili kuleta usawa na wanawake kuendelea kujiamini na kutumia fursa zilizopo kujiwezesha kiuchumi na kisiasa.

Alisema kila Machi 8 kila mwaka ni Siku ya Wanawake Duniani ambapo dunia inalenga katika kutambua utu, nafasi na mchango wa mwanamke katika maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa duniani.

Umoja wa Mataifa uliridhia na kuanza kuadhimisha siku hiyo mwaka 1975 kwa lengo la kukumbusha dunia juu ya usawa wa kijinsia na haki za wanawake, uamuzi ambao ulifikiwa ili kupinga mfumo dume ambao ulizikabili jamii mbalimbali duniani kote.

"Katika maadhimisho ya siku hii muhimu, THBUB inaungana na jamii na wadau mbalimbali duniani kutambua mchango wa wanawake katika jamii mbalimbali za maendeleo," alisema.

Kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka huu ni "Wanawake wasichana 2025:Tuimarishe haki, usawa na uwezeshaji" ambayo inatambua kuhusu wajibu wa jamii kuona umuhimu wa ujumuishi wa wanawake na wasichana katika mipango yote ya maendeleo,kusimama kidete kuhakikisha wanapata haki zao na fursa sawa katika nyanja zote za maendeleo.

Alisema kupitia kauli mbiu hiyo jamii pia inapata fursa ya kujadili na kuandaa mikakati madhubuti itakayosaidia kutatua changamoto zinazowakabili wanawake wasichana na makundi mengine yenye mahitaji maalum, zikiwemo zile zinazotokana na ukatili wa kijinsia ili kuleta usawa.

Rashal Energies kujenga vituo vya kujazia gesi

NA FATUMA KITIMA, DAR ES SALAAM

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amefanya mazungumzo na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Rashal Energies, Farhiya Warsame, inayojenga bomba la gesi kutoka Kisemvule hadi Mbagala lenye urefu wa kilomita 19 jijini Dar es Salaam.

Kampuni hiyo pia itajenga vituo vitano vya CNG kwa ajili ya kujaza gesi kwenye magari na viwanda huku lengo likiwa ni kufikisha zaidi ya vituo 30.

Mazungumzo hayo yalifanyika jana jijini Dar es Salaam, wakati wa kongamano na maonesho ya petroli ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPCE'25) yanayofanyika kwa siku tatu jijini humo.

Alisema lengo la serikali ni kuwa na mtandao mkubwa wa mabomba ya gesi pamoja na vituo vya kujazia gesi kwenye magari ili kuwezesha wananchi kupata huduma kwa urahisi.

Aliongeza kuwa serikali ipo tayari kutoa ushirikiano kwa kampuni zinazotaka kuwekeza katika kutoa huduma hiyo kwa wananchi.

Nae Farhiya Warsame, alimshukuru Dk. Biteko kwa miongozo yake ambayo imesaidia kampuni hiyo kuanza kutekeleza mradi huo.

Pia alilihukuru Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Serikali ya Tanzania kwa jitihada kubwa katika kuhakikisha mradi huo unakamilika.

Alisema kampuni hiyo imefanya utafiti wa kina kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi huo na imefuata taratibu na sheria zote za nchi ikiwa ni pamoja na kupata vibali vinavyohitajika.

Alisema baada ya kukamilika ujenzi wa bomba hilo kutakuwa na kituo cha Rashal Energies cha kujaza gesi gari, ikiwa ni pamoja na kuhudumia mabasi ya mwendo kasi.

"Rashal Energies pia itajenga vituo zaidi ya 30 vya kujaza gesi asilia, mtandao wa mabomba ya gesi kwa ajili ya gari, bajajina pikipiki pamoja na kusambaza gesi viwandani," alisema Farhiya.

Ujenzi wa bomba hilo, Unatarajiwa kuanzisha ajira zaidi ya 300 za moja kwa moja, na zaidi ya 200 zitapatikana baada ya kukamilika kwa vituo.

Vilevile alisema katika kuunga mkono juhudi za serikali, Rashal Energies itaanzisha huduma ya kujaza gesi kwa matumizi ya nyumbani ili kuwarahisishia wananchi kupata huduma hiyo kwa urahisi zaidi.

Alisema Rashal Energies ni kampuni yenye makao makuu jijini Dar es Salaam inayomilikiwa na kuendeshwa na Watanzania wazawa, huku ikiajiri wataalamu kutoka nchini.